Canada ,ndio nchi ya pili kwa ukubwa wa nchi kavu duniani ikifuata Russia ,iko katika bara la Amerika kaskazini na mpaka wa kusini wa nchi ya Canada ni nchi ya U.S ama ukipenda United States.Canada ni nchi iliyo upwekeni na (mpaka wake ni kilomita 8,893 kwa urefu) hupakana na U.S kwa nchi kavu pekee.

Ugonjwa wa UKIMWI

Reti ya kusambazwa kwa ukimwi Canada ni asilimia 0.3 na hiyo ndio nchi ya 89 kwa 168 zikilinganishwa kwa reti ya kusambazwa kwa ukimwi.Kwa watu milioni 34 wanaoishi Canada leo,kwa kukisia 63,604 wako na virusi vya ukimwi.Kwa hao ,59,522 ni watu waliopita miaka 15 na kuendelea.Ukitumia jinsia,asilimia 83.a ya hawa ni wanaume na asilimia 16.9 ni wanawake(*Novemba 1 st,1985 HADI June 30th,2007)*

Idadi ya kesi za usambazaji wa ukimwi kwa mwaka ilipunguka hadi ikafika 2,104 (mwaka wa 2000) halafu ikaanza kuongezeka tena.Kwa kesi zote zilizoripotiwa wale waliopata ukimwi zaidi ni wanaume walioshiriki katika ngono ya mume kwa mume na asilimia 41.2 na wa pili ni wale wanaotumia madawa ya kulevya na asilimia 22.8 (kulingana na shirika la afya ya umma la Canada Juni 2007).Kwa wanawake wale waliopata ukimwi zaidi ni wale wanaotumia madawa ya kulevya(kwa kutumia sindano moja kujidunga madawa hayo) na asilimia 41.1 na wa pili ni wale wanaoshiriki katika ngono ya mume kwa mke na asilimia 21.9.

Katika wilaya 13 za Canada ,zile nne kubwa kabisa(Ontario,Quebec,British Columbia na Alberta) zina asilmia 94.3 ya wale walio na virusi vya ukimwi katika nchi hiyo.Asilimia 81.7 ya Wacanada walio na virusi ni wazungu(ngozi yao ni nyeupe)

Nambari hizi zinaonyesha kuwa wanaume wazungu(wenya ngozi nyeupe) wanashiriki katika ngono ya mume kwa mume.

Hatua za serikali

Katika mwez i wa Oktoba 2005,serikali ilileta plani ya miaka tano inayoitwa *"KUISHI PAMOJA:CANADA KUPAMBANA NA UKIMWI"*(2005-2010).Canada inatambua haja ya kupambana na ukimwi nchini hiyo na pia duniani na ni moja ya sera za plani hii.Sera zilizowekwa katika orodha ya yatakayofanywa ni mifano ya hatua zinaofaa kuchukuliwa ili kupunguza ueneaji wa virusi vya ukimwi.

Plani hii ya kitaifa imepanga hatua tano katika sera zao zikiwemo:kuelimisha watu,kuhusisha dunia nzima ,kukagua na kuripoti,kuindelza mpango huu siku zaijazo na kupitisha habari kutumia mdomo.

Mipango hii ya Canada inalenga mambo yanayokumba dunia kwa sababu ya ukimwi yakiwemo:kupambana na kutengwa kwa wale walio na virusi vya ukimwi ,kurahisisha kupimwa na kutibiwa kwa ukimwi na njia za kuzuia kusambazwa kwa ukimwi na kuendelea kutafuta tiba thabiti ya ukimwi.Ni muhimu kuendelea kuelimisha umma ,katika survey iliyofanywa asilimia 17 ya Wacanada walisema kuwa ukimwi ukitibiw mapema <unaweza ponywa.(*KUISHI* PAMOJA)

Canada imechangia katika utafiti wa ukimwi duniani.Mwaka wa 2003 shirikisho la afya la Canada na shirikisho la maendeleo ya kimataifa la Canada na vikundi vingine kama UNAIDS lilileta Warsaw declaration ambayo ilipanga kupambana na usambazaji wa ukimwi kwa wale wanaotumia madawa ya kulevya .Canada pia imesaidia United Nations General Assembly Special Session(UNGASS) katika mambo yanyohusu ukimwi.

Waaborigini (kabila fulani ya Canada)

Kulingana na shirikisho la afya la Canada ,Waaborigini (Inuit na First nations) ni asilimia 3 ya wakaazi na wao ndio asilimia 15.4 ya kesi za ukimwi zilizoripotuiwa mwaka wa 2007 ,Juni .Hii haijumuishi watu 70 ambao kabila zao hazikurippotiwa.

Sababu za reti kubwa ya Waaborigini kuwa na ukimwi ni umaskini,utumiaji wa madawa ya kulevya kwa wingi na kutumia pombe,kuadimika kwa watu wanaochunga afya ya watu(madktari,mahospitali n.k) na kupunguka kwa utamaduni.Miaka iliyopita vikundi Fulani vimetokea ili kupambana na mashida yanayokumba Waaborigini.Baadhi ya vikundi hivi ni branchi za serikali kama First nations ya shirikisho la afya la Canada ,branchi ya afya ya Innuit na shirikisho la afya ya umma ya kikundi cha Waaborigini cha kitaifa huko Canada cha ukimwi.Makundi mengime yaliyomo ni kikundi cha Waaborigini cha Canada cha ukimwi ,ambacho ni kikundi kisicho na lengo ya kibiashara(hakitaki faida)

Majelani

Kama kulivyo katika mataifa mengine , kuna reti kubwa ya kusambazwa kwa ukimwi ndani ya majela kuliko nje ya majela .Hata kama matumizi ya dawa za kulevya ndani ya majela yamekataliwa na sharia kuna wafungwa ambao hutumia madawa ya kulevya wakiwa jelani.

Canada haina mfumo ule wa kubadilishia watumiaji wa madawa ya kulevya sindano na mfumo umesaidia kupunguza usambazaji wa ukimwi miongoni mwa watumiaji wa madawa ya kulevya katiki nchi nyingine kama vile Switzerland.Utetezi ni kuwa mfumo huo utaendeleza ama kueneza matimizi ya madawa ya kulevya.

Njia ya tatu ya usambazaji wa ukimwi majelani ni kupitia vitendo vya ngono.Hakuna njia ya kujua kwa hakika ni wafungwa wangapi wanaoshiriki katika vitendo vya ngono wakiwa jela,lakini wadadisi walikhisia kuwa inaweza kuwa asilimia 6(mwaka wa 1995).Kuna jela zingine ambazo ziko na kondomu za matumizi ya wafungwa lakini nyingi hazina.

*(Habari kuhusu majela imetoka kwa AIDS Calgary Awareness Association na HIV/AIDS Legal Network ya Canada)

Kujuza wasiojua

Miaka ambayo imepita uso wa ukimwi umebadilika,lakini kuna mambo kuhusu ukimwi ambayo hayajaweza kubadilika hata!Kuna watu ambao bado wanaamini kuwa ukimwi ni ugonjwa wa Waafrika

ama ni ugonjwa wa wanaume gay .Ukimwi ni ugonjwa wa kimataifa usiotambua rangi ya ngozi ya mtu ,kabila,miaka, ama uume au uke wa mtu.

Hata kama ukimwi haujaathiri watu Canada kama unavyoathiri watu Afrika ,ugonjwa huo bado unazidi kusambazwa.Wagonjwa wa ukimwi bado wanendelea kutengwa na jamii.Woga unazuia watu kupimwa na hata kusaka matibabu ambako kunaendeleza kusambaa kwa ugonjwa huu.

Kumaliza Ukimwi kabisa

Canda imechukua hatua muhimu sana mbele kwa kutambua kuwa ukimwi sio shida iliyomo nchini mwao pekee yake.Ili kupambana na kusambaa kwa ukimwi Canada ukimwi unafaa umalizwe duniani nzima kwanza.Hili ni muhimu sana kwa Canada hupata watalii na wahamiaji walio na ukimwi kutoka nchi nyingine.

Umaskini ni moja ya mambo muhimu yanayoongezea kusambazwa kwa ukimwi.Wale wasiopata chakula cha kutosha na chenye kumpa mtu afya nzuri ndio hujihusisha na madawa ya kulevya ama kuwa virukanjia ama malaya ukipenda.Uelimishaji wa umma unahitajika ili kutoa watu hawa hatarini ya kuupata ugonjwa wa ukimwi.

Elimu ndio moja muhimu ya kuzuia kusambazwa kwa ugonjwa wa ukimwi.Watu wanafaa kuelimishwa kuhusu vile ambavyo virusi vya ukimwi husambazwa,na hatua zile ambazo zinafaa kuchukuliwa ili kupunguza hatari ya kupata ukimwi.

Kupimwa mapema ni muhimu ili kuzuia usambazaji wa ukimwi bila watu kujua kwa wale wanaoshiriki katika ngono pamoja na kutumia sindano moja katika utumizi wa madawa ya kulevya.Kugundua kwamba una ukimwi mapema pia huwezesha mtu kupata matibabu ya ARV(Anti-Retroviral) mapema .

Ili kuzuia usambazaji wa ukimwi katika majela,na miongoni mwa watumizi wa madawa ya kulevya, serkali ya Canada na serekali za nchi nyingine zinafaa kukubaliana kuhusu ubadilishaji wa sindano za watumizi wa dawa za kulevya.

Mwishoni,uwasilishaji wa madaktari na mohispitali yasiyo ya bei ghali kwa umma diko kutapunguza reti ya usambazaji wa ukimwi hadi ufike asiliimia 0 na kupatikana kwa tiba na kingo dhabiti ya ukimwi.